

## Kanuni ya Matumizi Yanayokubalika

Wilaya inatambua kwamba uwepo wa teknolojia kwa shule huwapa wanafunzi nafasi kubwa kusoma, kuhusika, kuwasiliana, na kuimarisha ujuzi utakaowatarisha kwa kazi, maisha, na uraiya. Tumeazimia kuwasaidia wanafunzi kupata ujuzi wa teknolojia na mawasiliano utakaohitajika katika karne ya 21. Kwa hivyo, tunawezesha uwepo wa teknolojia kwa matumizi ya kielimu kwa wanafunzi na wafanyikazi. Hii Kanuni ya Matumizi Yanayokubalika- Acceptable Use Policy (AUP)- inaguzia mipaka na matarajio ya hayo matumizi kwa wanafunzi, waalimu, na wazazi wanapotumia teknolojia za shule au kwa vyombo wanavyomiliki kibinafsi ndani ya mali ya Wilaya/Eneo (District) la mashule.

### **Kazi na Majukumu ya Wafanyikazi**

Wilaya inaamini kuwa matumizi ya teknolojia inawabidi watumizi wote kuwa raiya dijitali walio salama na kuwajibika. Kwa hivyo, Wilaya itatumia mbinu zifuatazo kuhakikisha usalama wa watumizi.

- Mafunzo ya usalama mtandaoni (Internet) na uraiya dijitali yatafanyika kila mwaka.
- Waalimu na wafanyikazi watasimamia matumizi ya teknolojia yaliyokubalishwa kwa wanafunzi ndani ya madarasa kwa njia ya kuendelea.
- Uwepo wa Internet utawekewa vikwazo kulingana na kanuni za serikali ya jimbo na taifa na sera za Wilaya. Matumizi ya mtandao yanaweza kuchunguzwa na kurekodiwa wakati wowote.
- Wasimamizi wa shule na wale wa mtandao wanaweza kuchunguza faili na mawasiliano kuhakikisha matumizi yanayofaa.

### **Kazi na Majukumu ya Wazazi/Wasimamizi**

Wilaya inategemea wazazi/wasimamizi kushirikiana nasi kuwafunza wanafunzi kutumia teknolojia iliyopo kwa usalama na uwajibikaji. Ingawaje Wilaya itafanya kila juhudi kuzuia matumizi yasiyofaa, haiwezekani kuzuiya kila kitu kisichofaa. Vile vile, kina chochote kisichotumia waya (wireless connection) na kisichotunzwa na Wilaya hakisimamimiwi na kwa hivyo ni jukumu la mzazi/msimamizi.

### **Kazi na Majukumu ya Wanafunzi**

Uwepo wa teknolojia na mtandao umekusudiwa kuunga mkono malengo ya kielimu na mafundisho pekee. Wanafunzi wanatarajiwa kutumia raslimali kwa njia wajibifu na watachukuliwa hatua kulingana na tabia na mawasiliano yao. Mawasiliano yote, data na faili zinazohifadhiwa au kusambazwa kupitia mtandao wa Wilaya yanachukuliwa kuwa kama mali ya Shule za Umma za Kata ya Fayette na yanaweza kuchunguzwa na/au kuondolewa. Kwa mujibu wa hekima na mipaka ya kisheria, uhuru wa kunena na kuweza kupata habari utaheshimiwa.

### **Mifano ya Matumizi Yanayokubalika ni pamoja na (lakini kuna zaidi):**

- Fuata matarajio ya kitabia ya shule na ya Wilaya ya kuwa na heshima na raiya dijitali anayewajibika.
- Tumia raslimali za mtandao (pamoja na barua pepe) kama ilivyofundishwa kwa sababu za kielimu.
- Hifadhi na sambaza mambo mwafaka.
- Tumia teknolojia ya shule na/au ya kibinafsi wakati na kwa sababu zilizoidhinishwa pekee.

### **Mifano ya Matumizi Yasiyokubalika ni pamoja na (lakini kuna zaidi):**

- Pata, tuma na/au poka kwa njia maksudi, mambo yoyote yasiyofaa, yanayotusi, yanayosumbua, au ya aina ya matusi ama yale yanayochangia ghasia au vitendo vya uhalifu/uvunjaji sheria.
- Haribu kimaksudi raslimali duni au kuzitumia kwa sababu zisizo za kimasomo – (uhifadhi wa faili, uchapishaji, bandwidth)
- Tumia ama sambaza jina-siri au pasiwadi ya mtu mwingine, au ruhusu watu wengine kutumia jina-siri lako na pasiwadi.
- Dunisha/dhoufisha mtandao na viegezo vyake kwa njia yoyote ile – (uvunjaji (hacking), spamming, bypassing security, n.k.)
- Tumia mtandao wa shule kujifaidisha, kujitumbuiza, kuchangia siasa au shughuli zisizohusiana na shule.
- Kiuka sheria za uchapishaji (copyright) au tumia kazi ya mwingine bila ruhusa (plagiarism), pamoja na kupiga chapa software, muziki au faili zingine zinazosimamiwa na copyright.

- Haribu au iba kwa maksudi mali ya Wilaya au mali inayosiana na teknolojia ya mtu binafsi.
- Jihusishe na ukereshaji mtandaoni (cyberbullying), uchokozi, au tabia isiyo ya heshima dhidi ya wengine.

### **Kiukaji za Sera ya Matumizi Yanayokubalika**

Wanafunzi wanaokiuka AUP wanakabiliana na zilezile hatua za kinidhamu zilizokubaliwa na kuwekwa kwa Kanuni za Kukidhi Tabia ya Wanafunzi (Student Code of Conduct) kwa tabia sawa na tabia nje ya mtandao na ziko ndani ya amri ya wasimamizi wa shule.

### **Vifaa Vinavyomilikiwa Kibinafsi**

Wanafunzi watakaonyesha uraia mwema wa kidijitali na wana AUP iliyotiwa sahihi wanaweza kukubaliwa kutumia mtandao wa Wilaya kwa vifaa wanavyomiliki kibinafsi. Matumizi ya aina hiyo yatasimamiwa kama ilivyofafanuliwa hapa juu na yatabidi wanafunzi kutumia vifunguo spesheli walivyopewa na Wilaya kutumia vifaa vyao. Hata hivyo, udumishaji na utunzi wa hivyo vyombo utabaki kuwa jukumu ya jamii. Wilaya haina jukumu lolote kuhusu uharibifu au upotevu utakaotokana na matumizi ya vifaa vya kibinafsi katika eneo la shule. Wanafunzi wanatarajiwa kutumia vifaa kwa sababu mwafaka na nyakati zinazofaa.

Ingawaje matumizi ya vifaa katika mtandao wa Wilaya yanachunguzwa, wanafunzi na wasimamizi wa watoto chini ya umri wa miaka 18 wana jukumu la kuamua na kuwasilisha viwango ambavyo watoto wao wanafaa kufuata wanapotumia media na habari kutoka sehemu fulani na fulani. Vile vile, wanafunzi na wasimamizi wana jukumu la kuamua mambo ambayo wanafunzi wanayoweza kuona au kufikia wanapotumia mitambo nje ya ile ya Wilaya.

### **Idhini ya Kuwaruhusu Wanafunzi Fufungua Akaunti Mtandaoni za Web 2.0 Resources**

Kama sehemu ya mafunzo, wanafunzi wanaweza kutumia kurasa tofauti za mtandao (websites) kwa sababu za kimasomo juu ya raslimali zinazotolewa na shule kubuni vitu vinavyojulikana kama 'online word clouds', 'interactive pictures', 'infographics', maonyesho na miradi mingine ya kidijitali. Mingi ya hizi kurasa za masomo huhitaji akaunti za wanafunzi. Wakati mwingine, waalimu wa wilaya wanaweza kuwafungulia wanafunzi akaunti lakini si kila mara. Sheria inayojulikana kama 'Children's Online Privacy Protection Act (COPPA)' inahitaji kuwa kila mtoto chini ya umri wa miaka 13 kupata ruhusa ya mzazi kabla ya kufungua akaunti katika kurasa fulani za Web 2.0. Kwa kutia sahihi kwa hii barua, unasema kuwa umemruhusu mtoto wako kufungua akaunti katika sehemu fulani zilizotambuliwa na mwalimu kwa sababu za kimasomo. Sehemu ambazo waalimu wanatumia pamoja na wanafunzi ni lazima ziwe zimedhihirishwa na Wilaya, na ni lazima ziwe zinakubaliana na sheria hizi: KRS 61.931; KRS 61.932; KRS 61.933.

### **Idini/Ruhusa ya Matumizi**

*Kwa kusahihisha hii fomu, unakubali kuwa haki za mwanao kutumia raslimali za kielektroniki zinazotolewa na Wilaya na/au Idara ya Elimu ya Kentucky (Kentucky Department of Education (KDE)) ziko chini ya kanuni na vikwazo vilivyojumuishwa katika sera/hatua za Wilaya. Data iliyohifadhiwa kuandamana na huduma kama hizo inasimamiwa na Wilaya kwa mujibu wa sera 08.2323 na hatua zinazoandamana nayo. Pia unaelewa anwani ya barua-pepe anayopewa mwanao inaweza kutumiwa kupata huduma zingine za kielektroniki au teknolojia ambazo zaweza kuwa zimedhaminiwa ua hajizadhaminiwa na Wilaya, zinazoweza kuwa na huduma kama uhifadhi mtandaoni, mawasiliano mtandaoni na ushiriki mtandaoni, na usambazaji wa ujumbe wa mara moja (instant messaging). Utumizi wa hizi huduma unasimamiwa na kanuni za kawaida za wanannchi au zile za makubaliano ya kawaida. Data inayohifadhiwa katika hii mifumo, kama inavyowezekana, yanaweza kusimamiwa kufuatana na kubaliano baina ya KDE na watwaji huduma rasmi au baina ya mtumizi wa mwisho na mtwaji wa huduma. Kabla ya mtoto wako kutumia huduma mtandaoni, ni lazima akubali masharti ya huduma, na katika hali zingine, ruhusa yako wewe.*

---

Kama mwanafunzi wa Shule za Umma za Kata ya Fayette, ninaelewa na ninakubali kufuata kanuni kama zinazopatikana katika Kanuni za Matumizi Yanayokubalika hapa juu.

---

Sahihi ya Mwanafunzi

---

Jina la Mwanafunzi

---

Tarehe

Shule: \_\_\_\_\_

Darasa: \_\_\_\_\_

Kama mzazi/msimamizi wa huyu mwanafunzi, ninaelewa na kukubali kutii Kanuni za Matumizi Yaayokubaliwa kama yalivyotajwa hapa juu na kuguziwa katika sera ya bodi ya 08.2323 pamoja na taratibu andamanaji (zinazopatikana hapa [www.fcps.net](http://www.fcps.net)). Ninaelwa kuwa hili kubalio litabaki mpaka ule wakati mwanafunzi atakoma kuwa mwanafunzi wa shule za FCPS ama nikilitupilia mbali kwa kuandika barua.

---

**Sahihi ya Mzazi**

**Jina la Mzazi**

**Tarehe**

ILANI: SHERIA YA TAIFA INAHITAJI WILAYA KUCHUNGUZA SHUGHULI ZA WATOTO CHINI YA MIAKA 18 MTANDAONI.